

NOTISI YA MKUTANO NA KUTHIBITISHA AJENDA

TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA NNE

1. Taarifa inatolewa kuwa Mkutano **Mkuu wa Mwaka wa Nne** wa Mwalimu Commercial Bank Plc utafanyika katika Ukumbi wa **ISIKE MWANAKIYUNGI – Tabora Mjini** siku ya **Alhamis, Agosti 13, 2020 kuanzia saa 5:00 Asubuhi**
2. Ajenda ya Mkutano ni kama ifuatavyo:
 - 2.1 Kufungua Mkutano
 - 2.2 Kupitishwa kwa Ajenda.
 - 2.3 Uthibitisho wa Kumbukumbu za Mkuu wa tatu wa Mwaka 2019
 - 2.4 Kujadili Yatokanayo kwenye Mkutano Mkuu wa tatu wa mwaka 2019.
 - 2.5 Taarifa ya Mwenyekiti
 - 2.6 Kupokea Ripoti ya Wakurugenzi na kupitishwa kwa taarifa za Hesabu za Fedha za Mwaka 2019.
 - 2.7 Gawio
 - 2.8 Kuongeza mtaji wa benki
 - 2.9 Uteuzi wa wakurugenzi huru
 - 2.10 Ada za Wakurugenzi
 - 2.11 Uteuzi wa Wakaguzi wa nje.
 - 2.12 Mapendekezo ya Marekebisho ya MEMARTS.
 - 2.13 Mengineyo yatokanayo na mkutano.
 - 2.14 Tarehe ya mkutano ujao.
 - 2.15 Kufungwa kwa Mkutano.
3. Mwanahisa yeyote ambaye anataka kuingiza pendekezo lake katika kipengele cha 2.13 hapo juu lazima atoe taarifa kwa

maandishi siku tatu (3) kabla ya Mkutano Mkuu wa Mwaka.

4. Mwanahisa atakaeshindwa kuhudhuria ana haki ya kuteua mwakilishi kuhudhuria mkutano kwa niaba yake. Taarifa hizi zimfikie Katibu angalau saa arobaini na nane (48) kabla ya wakati wa mkutano.
5. Wanahisa wote wanaombwa kuja na vyeti vya hisa pamoja na vitambulisho siku ya mkutano.
6. Makabrasha ya mkutano yanapatikana kwenye matawi yetu ya Samora Avenue-na Mlimani Dar es Salaam, na katika ofisi zetu za Mwanza, Morogoro na Mbeya pia yatapatikana kwenye ukumbi siku ya mkutano.
7. Gharama za usafiri na malazi zitafanywa na wanahisa wenyewe

TAARIFA YA SEMINA KWA WANAHISA

Taarifa inatolewa kwamba kutakuwa na Semina kwa Wanahisa itakayolenga kutoa elimu kuhusu **“Hisa”, Elimu ya Fedha** na **Bidhaa zinazotolewa na Benki ya Mwalimu**. Semina hiyo itafanyika **Alhamis, tarehe 13/08/2020** katika Ukumbi wa **ISIKE MWANAKIYUNGI Hall -TABORA** kuanzia saa **3.00 asubuhi**.

